

Maswali

1. Waisraeli walifanya kazi gani Misri?
2. Mungu alimwambia Musa awapeleke watu wapi?
3. Waisraeli walienda na vitu gani?
4. Mungu aliwaonyeshaje pakuenda?
5. Mbona Waisraeli waliogopa walipoona Farao?
6. Mbona Musa hakuogopa?
7. Nini ilifanyika wakati Musa alinyosha fimbo juu ya bahari?
8. Mungu aliwalinda Waisraeli namna gani usiku?
9. Waisraeli walivuka bahari salama?
10. Wamisri walivuka bahari salama?

Majibu

1. Walitengeneza matofali na kujenga miji.
2. Nchi yao yenyeye Mungu alikuwa amewaaahidi.
3. Waisraeli walichukua nguo, vyombo, vyakula na mifugo, hata dhahabu kutoka kwa Wamisri.
4. Wingu kubwa mrefu mchana na nguzo ya moto usiku.
5. Walifikiria Farao atawarejesha Misri .
6. Musa aliamini kwamba Mungu atawaokoa.
7. Mungu alifanya upepo wa nguvu ukavuma na kukausha katikati ya bahari.
8. Mungu aliweka wingu mrefu katikati ya Waisraeli na Wamisri.
9. Waisraeli walivuka salama.
10. Wamisri walizama baharini.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 1

17 Kuvuka Bahari ya Shamu

Marejeo

Kutoka 14 : 5-31

Kiini cha somo

Kuonyesha vile Mungu analinda watu wake wanaomwamini

Maneno maalum

1. Watumwa + Misri + Farao + tauni kumi + Pasaka + kutoka Misri.
2. Wingu kubwa mrefu + Bahari ya Shamu
3. Farao+ kuwarejesha + Bahari ya Shamu
4. Waisraeli + uoga
5. Mungu atasaidia + fimbo + upepo + wingu + vuka + njia kavu pana.
6. Wamisri wanafuata
7. Zama + Mungu aliokoa + asante

17.1 Waisraeli walifanya kazi ya utumwa Misri. Walifanya kazi nydingi ya kutengeneza matofali na kujenga miji. Mungu alimwambia Musa awapeleke Waisraeli kwa nchi waliyoahidiwa. Mfalme wa Misri, Farao, hakutaka watumwa waende. Mungu aliwapiga na tauni kumi. Tauni ya mwisho ilifanywa na malaika aliyeua wazaliwa wa kwanza wa kila nyumba. Aliruka kila nyumba ya Mwisraeli aliyetii amri. Farao aliwaacha waende nchi yao. Taifa lote la Waisraeli lililokuwa kubwa, waliacha nyumba za Misri na kuenda. Waliondoka upesi kabla Farao hajabadilisha mawazo. Walichukua nguo, vyombo, vyakula na mifugo yao. Wamisri waliwapa vitu vingi vya dhahabu.

17.2 Hawakuenda safari ya haraka kwa ajili ya watoto wadogo na mifugo. Mungu aliwaongoza kwa njia ndefu. Mungu alikuwa nao. Kulikuwa na wingu kubwa ndefu mbele yao kila mchana na nguzo ya moto usiku. Walifuata hiyo wingu mpaka kwa Bahari ya Shamu.


17.3 Waisraeli walipoondoka Misri, Farao alikuwa na hofu juu ya wafanyakazi wa matofali na kujenga miji. Watumwa wake Waisraeli walikuwa wameenda. Farao aliamua kuwarejesha. Aliuja hawataenda haraka kwa ajili ya watoto na mifugo. Farao alikuwa na farasi na magari mengi ya kubeba jeshi lake. Kwa hivyo ataenda haraka sana. Farao na jeshi lake wakawafuata na kuwapata Waisraeli kwa Bahari ya Shamu.

17.4 Waisraeli walipoangalia nyuma, waliona Farao na jeshi lake wanakuja kuwachukuwa. Waliogopa. Hawangeweza kuhepa. Bahari ya Shamu ilikuwa mbele yao kwa hivyo hawawezi kuvuka maji. Farao alikuwa nyuma yao akija kwa haraka sana. Waliogopa kwa sababu walijua Farao atawarudisha Misri.

17.5 Musa aliwambia, "Msiogope, Mungu atatusaidia." Musa hakuogopa . Aliuja Mungu alikuwa akiwalinda. Aliwambia ya kwamba Mungu atawaokoa kutoka kwa wa Misri. Musa alisema ukweli. Mungu alimwambia kuelekeza fimbo kwenye bahari. Mungu alifanya upepo ukavuma juu ya bahari usiku kucha na kutengeneza njia pana kavu katikati ya bahari. Mungu aliwalinda usiku wote. Wingu kubwa mrefu ilifuata nyuma ya Waisraeli. Farao na jeshi lake hawangeweza kuwaona kwa ajili ya wingu. Hawakuona chenye kilikuwa kikiendelea.

Kulipokucha asubuhi, watu waliona hiyo njia pana kavu katikati ya bahari. Musa aliwaambia wavuke waende ng'ambo ingine ya bahari.

17.6 Wamisri walipoona njia, walifuata Waisraeli. Waisraeli walivuka salama upande mwingine wa bahari. Lakini Wamisri walikuwa bado baharini katikati kwa hiyo njia. Magari na farasi kadhaa yalikuwa yamegwama matopeni kwa hiyo njia. Wamisri waliogopa na kutaka kurudi nyuma.



17.7 Waisraeli walipovuka wote salama Musa alinyosha fimbo yake juu ya bahari. Mungu akaachilia maji irudi na kufunika hiyo njia. Wamisri wakazama kwa maji. Waisraeli waliona maji yakirudi wakajua wako salama. Walijua Mungu amewaokoa kutoka kwa Farao. Musa na Waisraeli walishukuru Mungu kwa kuwaokoa.